


# KUTUMA MAOMBI YA UI
## Mafao ya Bima ya Kutoajiriwa

### JE, NANI ANAWEZA KUPEWA MAFAO YA BIMA YA KUTOAJIRIWA?

Kama umeshawahi kufanya kazi New York unaweza kuwa na sifa ya kupewa mafao ya Bima ya Kutoajiriwa. Ni lazima uwe:

- Umepoteza ajira si kwa kosalako binafsi.
- Na mapato ya kutosha ya awali yatokanayo na ajira ili ufungue madai
- Tayari, na utayari na uwezo wa kufanya kazi mara moja
- Mtafutaji wa dhati wa kazi na utunze kumbukumbu (ya mtandaoni au ya maandishi) ya jitihada zako

Kama huna uhakika kama unafuzu, bado unaweza kutuma maombi mapema kadri iwezekanvyo. Sisi tutaamua kama una sifa. Kwa taarifa zaidi kuhusu kuwa na sifa, tafadhali angalia Sura ya 2 ya kijitabu chetu cha mdai kupitia **dol.ny.gov/unemployment-insurance-claimant-handbook**.

### JE, NATUMAJE MAOMBI YA MAFAO?

Njia ya haraka na salama zaidi ya kutuma maombi (kufungua madai) kwa ajili ya mafao ya Bima ya Kutoajiriwa ni kwenye tovuti yetu kupitia **https://unemployment.labor.ny.gov**.

Utahitajika kutumia NY.gov ID. Maelekezo ya kutengeneza NY.gov ID yapo katika ukurasa wa kuingia. Kama unapata tabu kutengeneza au kuifikia NY.gov ID yako, angalia maelekezo yenye picha kwenye ukurasa wa kuingia, tazama Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara ya NY.gov, au piga **800-833-3000** Jumatatu hadi Ijumaa, 8:30 am hadi 4:30 pm.

Unaweza kufungua madai mtandaoni:

- Jumatatu hadi Alhamisi 7:30 am mpaka 7:30 pm
- Ijumaa 7:30 am mpaka 5 pm
- Mwisho wa wiki kuanzia Jumamosi 12:01 hadi Jumapili 7:00 pm

Unaweza pia kufungua madai kwa njia ya simu ya bure kupitia **888-209-8124** kuanzia 8:00 am hadi 5:00 pm Jumatatu hadi Ijumaa. Bonyeza 9 kwa huduma za utafsiri wa lugha. Watumiaji wa TTY/TDD: mpigie muunganisha simu kupitia **800-662-1220** na mwombe akuunganishe na **888-783-1370**. Kwa video au watumiaji wengine wa huduma za kuunganishwa simu, wasiliana na muunganisha simu wako na mwombe akupigie **888-783-1370**.

### JE, NAHITAJI KUWASILISHA NINI?

- Nambari yako ya Usalama wa Kijamii (SSN)
- Leseni yako ya Udereva ya Jimbo la New York au nambari ya kadi ya Utambuzi wa gari (kama una yoyote ya hizo)
- Anwani yako kamili ya nyumbani na msimbo wa posta
- Nambari ya simu ambayo tunaweza kukupata kuanzia 8:00 am hadi 5:00 pm Jumatatu hadi Ijumaa
- Nambari yako ya kadi ya Usajili wa Mgeni (kama wewe si raia wa Marekani na una kadi)
- Majina na anwani ya waajiri wako wote kwa miezi 18 iliyopita, wakiwemo waliopo katika majimbo wengine
- Nambari ya Usajili wa Mwajiri au Nambari ya Serikali Kuu ya Utambuzi wa Mwajiri (FEIN) ya mwajiri wako wa hivi karibuni (FEIN ipo kwenye fomu zako za W-2)
- Nakala zako za fomu SF8 na SF50, kama ulikuwa mwajiriwa wa serikali
- Fomu yako ya utengano ya hivi karibuni (DD 214) kama ulikuwa jeshini

Unaweza kufungua madai bila ya nyaraka zote hizi. Hata hivyo, taarifa zinazokosekana zinaweza kuchelewesha malipo yako ya kwanza.

Kama huwezi kuchapisha kurasa za tovuti, hakikisha una kalamu na karatasi ili unakili taarifa husika.

Kama unafungua madai mtandaoni na unataka mafao yako yaingizwe moja kwa moja kwenye akaunti yako ya benki, utahitaji hundi ambayo imeandikwa nambari za msimbo wa benki na za akaunti ya hundi.

## JE, NAWEZAJE KUSAIDIWA KUFUNGUA MADAI?

Kama una ulemavu au tatizo la lugha na unahitaji msaada wa kufungua madai yako, rafiki au ndugu anaweza kukusaidia. Hata hivyo:

- Lazima uwe na msaidizi wako kila wakati anapokusaidia na kutumia PIN yako
- Unawajibika kwa matendo ya msaidizi wako
- Kama hautakuwepo wakati msaidizi wako anapokusaidia, unaweza kupigwa faini, ikiwemo kupoteza mafao yako

## JE, NAWEZAJE KUDAI MAFAO YA WIKI/ KUTOA UTHIBITISHO WA MAFAO?

Baada ya kufungua madai yako, unapaswa kudai mafao ya wiki kwa kila wiki unayoendelea kutokuwa na ajira. Unaweza kufanya hivi ama mtandaoni **https://unemployment.labor.ny.gov** au kupiga nambari yetu ya bure ya Tel-Service **888-581-5812**.

Wakati utakapodai mafao ya wiki, utaulizwa mfululizo wa maswali. Ni muhimu kuyajibu kwa ukweli, kwa kuwa unathibitisha kwa Idara ya Kazi kwamba majibu yako ni ya kweli na sahihi. Ndiyo maana mchakato huu unaitwa pia “Kutoa Uthibitisho wa Mafao.”

Kwa madhumuni ya Bima ya Kutoajiriwa, wiki inaanzia Jumatatu hadi Jumapili. Watu wengi wanadai mafao ya wiki kwa wiki iliyopita siku ya Jumapili. Hata hivyo, unayo nafasi hadi Jumamosi inayofuata kufanya hivyo.

Kisheria, wiki ya kwanza ya madai yako ni wiki ya kusubiri majibu. Hutapewa mafao katika wiki hii, lakini unapaswa kuwa tayari, kuwa na utayari na uwezo wa kufanya kazi na kutafuta kazi.

## JE, LINI NITAANZA KUPEWA MAFAO?

Ikiwa unastahiki na hakuna matatizo kwenye dai, kwa kawaida huchukua wiki tatu hadi sita kuanzia wakati unapowasilisha dai lako hadi unapopokea malipo yako ya kwanza. Hii ni kwa sababu tunapaswa kukagua na kushughulikia ombi lako.

## JE, NITAPEWAJE MAFAO YANGU?

Kama ulituma maombi ya Bima ya Kutoajiriwa kupitia mtandaoni, uliulizwa iwapo unataka kupokea mafao yako kwa njia ya benki au kadi ya benki. Kama ulituma maombi kwa njia ya simu, utapokea mafao yako kupitia kadi ya benki. Hatutoi tena mafao kwa njia ya hundi.

## TAARIFA ZA ZIADA

Baada ya kutuma maombi ya mafao, utapokea notisi kwa njia ya posta inayoitwa Monetary Benefit Determination (Azma ya Mafao ya Fedha). Tafadhal isome mara moja. Itakwambia iwapo unayo mapato ya kutosha ili kufuzu Bima ya Kutoajiriwa ama la. Itakwambia pia nini cha kufanya iwapo mapato yako yote hayakuorodheshwa kwenye notisi hiyo. Muhimu: Monetary Benefit Determination haisemi kwamba kwa hakika utapewa mafao. Inakwambia tu iwapo una mapato ya kutosha na umefuzu ama la. Kama utakidhi matakwa yote, mafao yako yataanza kutumwa. Kama utaonekana umekosa sifa, utapokea barua kutoka kwetu.

Unaweza kupoteza mafao kama hutosasisha anwani na nambari yako ya simu. Barua ya Bima ya Kutoajiriwa haitumwi kwa njia ya Ofisi ya Posta.

Rudisha madodoso yote mara moja ili stahiki yoyote ya madai yako isichelewe au isikataliwe.

## KWA MAELEZO ZAIDI

Angalia Bima ya Kutoajiriwa: Kijitabu cha Mdai kupitia **dol.ny.gov/unemployment-insurance-claimant-handbook** kwa taaarifa zaidi kuhusu mada zilizojadiliwa kwenye maelezo haya muhimu. Kijitabu hiki kitatumwa kwako kama utachagua kukipokea wakati wa kufungua madai yako.

Maswali yanayoulizwa Mara kwa Mara yapo kwenye tovuti yetu kupitia **dol.ny.gov/claimant-frequently-asked-questions**.

Kama una swali mahsusi kuhusu madai yako au maendeleo yake, tutumie ujumbe salama kupitia **https://unemployment.labor.ny.gov**. Ingia kwenye akauni yako ya mtandaoni na bofya ikoni ya barua sehemu ya juu kulia ya ukurasa wa My Online Services. Au, tupigie Kituo chetu cha Madai ya Simu kupitia **888-209-8124**. Jumatatu na siku baada ya sikukuu ya umma ni siku zenye shughuli nyingi sana kwa kupiga simu. Alhamisi na Ijumaa hakuna shughuli nyingi.



Idara ya Kazi ya Jimbo la New York ni Mwajiri/Programu anayetoa Fursa Sawa. Vifaa na huduma za usaidizi zinapatikana vikiombwa kwa watu wenye ulemavu.

NEW YORK STATE OF OPPORTUNITY. Department of Labor